

Public education
Discover a world of opportunities

NAMBA: KUSOMEA NYUMBANI

MAWAZO YA SHUGHULI ZA HESABU NYUMBANI

Kusoma pamoja

Vitabu ni njia rahisi na yafuraha ya kuleta hesabu nyumbani. Unaposoma, ongezea furaha kwenye mchezo kwa kuiliza maswali kama vile:
Ni nani alikuwa wa kwanza kufika? Ni watu wangapi wana nywele rangi ya udongo? Ni nani mrefu sana kwenye picha? Na tuko kwenye ukurasa upi? Hesabu kurasa wakati unazigeuza.

Zungumza kuhusu masaa

Msaidie mtoto wako kusoma saa zote mbili za kizamanina za kisasa. zungumzia kuhusu masaa.

Kwa mfano: *Je, kipindi chako cha television inachokipenda huanza saa gapi?*

Na inakaa kwa muda mgani?

Michezo

Michezo inahusu hesabu na huwa ni rahisi kuzungumzia. Uuliza maswali kama vile: *Timu imepata magoli mangapi? Timu inaongoza na magoli mangapi? Ni mchezaji mgani ameingiza magoli mengi?* Unaweza:

- Onyesha alama na nyakati zinavyo onyeshwa kwenye ubao
- Zungumzia michezo katika mbio - kwanza, pili, tatu ... mwisho
- Andika siku za michezo na nyakati kwenye kalenda na majadiliano juu ya siku za wiki, miezi yote ya mwaka na majira.

Chakula na kupika

Uuliza mtoto wako akusaidie kupima viungo na miiko, vijiko na vikombe, na kuangalia masaa ya kupikia. watie moyo kuinua vitu na kutofautisha ni kipi kizito. Wasaidie kufahamu jinsi vyakula na vinywaji vinawenza kuwa pamoja kwa usawa, kwa mfano kata sandwiches (mikate) au matunda katika nusu na kusema: *Nimekata hii katika vipande viwili sawa - nusu ni yenu na nusu ni yangu.*

Andaa chakula pamoja na uliza maswali kama:

- *Ni watu wangapi wanaokula?*
- *Tunahitaji masahani na vikombe vingapi?*
- *Je, unaweza ukupata masahani za kutosha bila kuhesabu kila sahani? Tunahitaji masahani sita, hizo ni tatu na zingine tatu.*
- *Kama tunahitaji vipande viwili nya mkate kwa kila sandwich, je kuna mkate wa kutosha kutengeneza sandwiches kwa kila mtu?*

Onyesha mtoto wako kwamba wingi wa jumla wa kundi la vitu haina mabadiliko hata kama ukipanga upya. Weka baadhi ya vitu katika mstari na uulize: *Ni ngapi? Weka vitu sawa katika kundi na uulize: Ni ngapi? Jibu ni sawa.*



Department of
Education

**Utakuta masomo zaidi kwenye
Vifurushi vy'a habari za nyumbani
kwenye education.wa.edu.au.**